# WADAU WAJADILI KUHUSU USANIFU MPANGO WA USAJILI WA MATUKIO MUHIMU YA BINADAMU NA UKUSANYAJI WA TAKWIMU

Serikali imedhamiria kuboresha Mfumo wa usajili wa vizazi, vifo na sababu zake, ndoa na talaka kupitia Mkakati wa kitaifa wa usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu unaojulikana kama ( National Civil Registration and Vital Statistics – CRVS –Strategy) ambao utakuwa muarobaini wa changamoto mbalimbali zinazochangia hali ya usajili kutokuwa ya kuridhisha na hivyo kama Taifa kukosa takwimu sahihi ya matukio hayo.

Waziri wa Katiba na Sheria Prof Palamagamba Kabudi akizungumza na wawakilishi na Viongozi wa Wizara hiyo,Taasisi, Idara mbalimbali za serikali na Wadau wa Kimataifa wa Maendeleo katika ufunguzi wa kikao cha wadau kuhusu usanifu Mpango wa usajili wa Matukio muhimu ya Binadamu na ukusanyaji wa takwimu kilichofanyika hii leo Mkoani Dodoma amesema tayari mchakato wa kurekebisha mfumo wa Sheria zinazosimamia masuala ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu umeshaanza ambapo Tume ya kurekebisha Sheria imeshakamilisha utafiti wake juu ya umadhubuti na dosari zilizopo katika mifumo ya kisheria hapa Nchini.

Wakati huo huo Prof Kabudi ameipongeza RITA kwa kuanza maboresho katika usajili na kuwapatia vyeti vya kuzaliwa Watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano katika Mikoa saba ambapo Mpango umefanikiwa kwa asilimia 77 huku Mikoa minne kati ya hiyo ikifanikiwa kwa asilimia 100 na hivyo kuthibitisha wazi kuwa iwapo maboresho makubwa yakifanyika kupitia Mkakati wa Kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya Binadamu na ukusanyaji wa takwimu kwa kiasi kikubwa Nchi itapiga hatua katika upatikanaji wa takwimu sahihi kwa ajili ya mipango mbalimbali ya Maendeleo.
‘’ Ni dhahiri kwamba mafanikio yaliyopatikana ni makubwa na yanatoa picha halisi ya kwamba tukirasimisha Mpango huu kwa mabadiliko ya mfumo wa kisheria tutafanikiwa kwa kiwango cha juu’’ amesema Prof Kabudi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya ushauri ya RITA Prof Hamis Dihenga amebainisha maeneo manne yaliyoonekana kuwa ni kikwazo kwa usajili wa vizazi,vifo na sababu zake ,ndoa na talaka ambayo ni Mfumo wa sheria na uthibiti na muundo wa kiutawala usiojitosheleza, Mfumo wa ukusanyaji takwimu ambao haujakamiliaka, pamoja na Ushiriki na uratibu wa wadau usioridhisha na hivyo kushauri katika maboresho yanayoendelea ni

lazima kuzingatiwe mfumo mpya utakaokuwa rafiki wenye kufikiwa na wananchi wengi kwa urahisi kwa kuzingatia wingi na mtawanyiko wa watu, jiografia ya nchi yetu, uoto wa asili, upatikanaji wa umeme na mawasiliano ya mtandao wa simu. Matumizi ya Tehama katika kurahisisha upatikanaji wa taarifa na kusaidia mfumo kufanya kazi.

Mpango wa maboresho Mfumo wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu (CRVS) Tanzania Bara, ulianza kwa kufanyika kikao cha maandalizi cha Kamati ya Ufundi kilichokaa tarehe 24 Aprili, 2014 Jijini Dar es Salaam.

Tathmini ilifanyika katika kanda zote za kitakwimu Tanzania Bara ambapo ilihusisha upitiaji wa nyaraka na kufika maeneo husika. Timu ya Tathmini ilikusanya taarifa kutoka kwa wasemaji wa ofisi za katibu tawala wa wilaya (DAS), vituo vya tiba, vituo vya polisi, taasisi za kidini, makatibu watendaji wa kata, viongozi wa vitongoji, wahudumu wa maeneo ya kuzikia, wahudumu wa nyumba za kuhifadhia maiti pamoja na watu binafsi katika wilaya. Watu walioshiriki katika tathmini ni: watumishi katika wizara, idara na wakala za serikali; wawakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Watoto (UNICEF); na kutoka taasisi zisizo za kiserikali.

Hayo yote yamefanyika kwa kuzingatia taratibu za Programu ya Afrika katika Kuongeza Kasi ya Kuboresha CRVS (Africa Programme on Accelerated Improvement of Civil Registration and Vital Statistics - APAI-CRVS) katika nchi zote za Afrika.